# UAINISHAJI WA KATEGORIA YA KIHUSISHI KATIKA LUGHA YA KISWAHILI

*Fokas Mkilima*
*Chuo Kikuu cha St John's cha Tanzania- Tanzania*
*mkilima2000@gmail.com*

**Ikisiri**

*Kategoria ya kihusishi katika lugha ya Kiswahili imeonekana kuwa na mkanganyiko katika uainishaji wake. Wanaisimu wameonekana kutofautiana kuhusu uainishaji wa kategoria hii. Baadhi ya wanaisimu wamekuwa wakiweka maneno ya kategoria ya kihusishi katika kategoria ya viwakilishi, vivumishi na viunganishi. Kutokana na mkanganyiko wa yapi ni maneno yanayoingia katika kategoria ya vihusishi, makala hii inabainisha maneno ya kategoria ya vihusishi ili kupunguza au kuondoa mkanganyiko juu ya kategoria ya vihusishi katika lugha ya Kiswahili. Utafiti huu ulitumia mbinu ya uchanganuzi wa nyaraka kutoka katika maandiko ya wanaisimu wa lugha za kigeni pamoja na wa Kiswahili. Uchanganuzi huo ulizingatia uainishaji wa kategoria ya vihusishi, aina za vihusishi, fasili, sifa na dhima ya vihusishi. Pia, mtazamo wa kisasa umetumika katika kubainisha kategoria ya vihusishi. Mtazamo huu unatumia kigezo cha kisintaksia katika kuainisha maneno kwa kuzingatia mtawanyiko wake, dhima kisarufi na mnyambuliko wa aina hii ya maneno. Vilevile, kigezo cha kimofolojia na kisemantiki kimetumika. Makala hii inatumia vigezo hivyo katika kubainisha kategoria ya vihusishi katika lugha ya Kiswahili.*

## 1.0 Utangulizi

Makala hii inaangazia kategoria ya kihusishi katika lugha ya Kiswahili. Kategoria ya kihusishi imeonekana kukanganywa na kategoria zingine za maneno kama vile viwakilishi, vivumishi na viunganishi na baadhi ya wanaisimu, kwa mfano, Matinde (2012) ameainisha aina mojawapo ya viwakilishi kuwa ni vya a-unganifu pia vivumishi vya a-unganifu ingawa mifano anayotoa ni ileile, yaani ya *cha la, wa, kwa, za* n.k. Nao Habwe na Karanja (2004) wanaeleza kuwa aina mojawapo ya vivumishi ni vivumishi vya a-unganifu. Mifano inayotolewa inafanana na ile inayotolewa na Matinde hapo juu. Kutokana na mkanganyiko huo imekuwa ni vigumu wakati mwingine kuelewa kategoria ya vihusishi inajumuisha maneno yapi. Mkanganyiko huo unatokana na sababu zifuatazo: kwanza, ni kutokana na baadhi ya wanaisimu wa Kiswahili kutokubaliana juu ya maumbo mwafaka ya vihusishi. Kwa mfano, katika uainishaji wa Kihore na wenzake (2008) kama walivyonukuliwa na Philipo (2012) wanatofautiana na wanaisimu wengine kwa kutoainisha vihusishi kama kategoria mojawapo katika maneno ya lugha ya Kiswahili bali maneno hayo yanachukuliwa kuwa ni viunganishi vihusishi. Pili, ni utokeaji na uamilifu wa maneno hayo katika tungo, yaani maneno yanayoambatana na vihusishi katika tungo na dhima zake. Tatu, ni tofauti ya vigezo vilivyotumika katika uainishaji wa maneno hayo; kwa mfano, Matinde (2012) ameonekana kutumia sana kigezo cha kisintaksia na kisemantiki wakati Kihore na wenzake (2008) wametumia kigezo cha kisemantiki. Hivyo, makala hii inalenga kubainisha kategoria ya vihusishi ili kuondoa mkanganyiko uliopo kwa kuonesha maumbo ya vihusishi, utokeaji wake pamoja na maneno mengine na vigezo vya uainishaji wake.

### 1.1 Uainishaji wa Maneno

Historia ya uainishaji wa maneno inaturejesha nyuma kipindi cha karne ya 5 KK ambapo kazi kubwa kuhusu taaluma ya lugha ilifanywa na wanamapokeo, hao ni wanaisimu walioanza kuchunguza sarufi za lugha. Wanamapokeo walifanya uchunguzi wa kiisimu kwa kuhusisha hasa lugha za Ulaya. Uainishaji wa maneno, kwa mara ya kwanza, ulifanywa na Mwanaisimu wa Kigiriki, Dionysious Thrax katika lugha ya Kigiriki. Tangu wakati huo hadi sasa, uchanganuzi wa lugha nyingi za Ulaya umejikita katika uainishaji wa aina nane za maneno ulioanzishwa na Dionysius Thrax. Wanaisimu waliofuatia wamekuwa ama wakiyapangilia upya au kuyagawanya zaidi maneno ambayo yalishaainishwa (Aussant, 2013). Dionysious Thrax (1874) kama anavyonukuliwa na Philipo (2012),

alichambua aina nane za maneno katika lugha, ambazo ni: nomino, kitenzi, kibainishi, kihusishi, kibadala (kiwakilishi), kielezi, kiungo (kiunganishi), na faridi pekee (neno lenye umbo na maana lakini haligawiki). Katika uainishaji wake, tunaona dhahiri kuwa kategoria ya kihusishi ilikuwapo. Katika lugha ya Kiswahili, wapo wanaisimu wengi waliobainisha kategoria ya vihusishi katika uainishaji wao. Mathalani, Nkwera (1978) na Kapinga (1983) kama wanavyonukuliwa na Massamba na wenzake (1999), Mgullu (1999), Habwe na Karanja (2004), na Matinde (2012).

Mgullu (1999) akiangalia mofolojia ya vihusishi anasema kuwa vihusishi vya Kiswahili huwa na mzizi pekee na haviambishwi ingawa wakati mwingine kihusishi “na” huambishwa; mfano, nalo, navyo, nao, nasi n.k. Mgullu (1999) anakiri wazi kuwa kazi ya vihusishi katika Kiswahili hufanywa zaidi na vikundi vihusishi. Usemi huu hauna mashaka lakini maneno tajwa hapo juu (“nalo”, “navyo”, “nao” na “nasi”) hayawezi kuambatana na maneno mengine yakaunda kikundi bali yanasimama kama neno moja na hivyo kupoteza uwezo wa kuunda kikundi.

Matinde (2012) akijadili aina za maneno katika lugha ya Kiswahili, anabainisha kategoria mojawapo kuwa ni viwakilishi. Anaendelea kufafanua kuwa viwakilishi ni maneno yanayosimama badala ya nomino. Katika kuchambua aina za viwakilishi, anasema kuwa moja ya aina hizo ni viwakilishi vya a-unganifu kama inavyoonekana katika mifano ya viwakilishi vya a-unganifu vilivyotolewa katika tungo zifuatazo:

a. Mtoto **wa** jirani amefukuzwa.
b. Kalamu **ya** Patrick ni nzuri **ya** Amina haina ubora.
c. **Ya** Kigali ilipendeza kuliko **ya** Nairobi.
d. Kiko **cha** baba kimezima.
e. Jogoo **wa** shamba hawiki mjini.
   **Chanzo:** Matinde (2012: 134)

Tukitazama mifano ya tungo a, b, d na e, tunaona kuna upungufu. Ikiwa viwakilishi ni maneno yanayosimama badala ya nomino, tunaona wazi maneno hayo hayasimami badala ya nomino kwa kuwa nomino hizo zipo. Katika muundo wa sintaksia ya lugha ni vigumu kuwa na mfuatano wa nomino na viwakilishi pamoja. Hivyo, maneno hayo hayana sifa ya kuwa viwakilishi bali ni vihusishi. Pia, katika mfano wa c, “**ya”** haiwezi kuwa kiwakilishi hata tukijiuliza kiwakilishi hicho kinasimama badala ya nini, jibu lake si jepesi kueleweka. Pengine, jibu tutakalopata linaweza

kudhaniwa kuwa ni nomino fulani, lakini nomino hiyo haiwezi kusimama katika nafasi hiyo bali nomino na kihusishi "ya" vitafuatana na sio kubadilishana nafasi. Jambo hilo linajitokeza pia katika uainishaji wa vivumishi (vivumishi a-unganifu). Tazama tungo zifuatazo:

a. Mtoto **wa** mfalme;
b. Kiatu **cha** yule binti kimeibwa;
c. Jeneza **la** Wanjara limechomwa;
d. Vilio **vya** watoto vimetulia.
**Chanzo:** Matinde (2012: 135).

Tunatambua dhima ya vivumishi ni kuipambanua nomino. Tunapotazama miundo inayopewa sifa ya vivumishi katika tungo hizo, tunabaini upambanuzi wa nomino unafanywa kwa kuhusishwa na nomino nyingine. Kutokana na dhima hiyo, hatuoni sababu ya moja kwa moja ya kuyaweka maneno hayo katika kategoria ya vivumishi badala ya vihusishi. Jambo hilo tunaliona pia kwa Habwe na Karanja (2004) wanapobainisha aina za vivumishi, wanasema kuna vivumishi vya a-unganifu; mfano wa a-unganifu wanadai kuwa ni viunganishi vinavyoundwa kwa kiambishi -a ambacho ni aina ya kiambishi tamati kinachoambishwa kwenye kiambishi ngeli kwa ajili ya kuleta maana inayotakiwa kwenye upatanisho wa kisarufi baina ya makundi mbalimbali ya maneno. Tunapochunguza maneno hayo tunaona hayafai kuwa katika kategoria ya vivumishi bali yanaingia katika kategoria ya vihusishi.

a. Mtoto **wa** Njoroge amevaa vizuri.
b. Meno **ya** tembo ni ya thamani kubwa.
c. Kitabu **cha** sarufi kimepotea.
d. Mti **wa** maendeleo humwagiwa jasho badala ya maji .

**Chanzo:** Habwe & Karanja (2004:186)

Hata hivyo, kuna wanaisimu wa Kiswahili ambao katika uainishaji wa maneno hawajabainisha kuwa vihusishi ni mojawapo ya kategoria katika lugha ya Kiswahili. Miongoni mwao ni Kihore (1996b), na Massamba na wenzake (1999), Massamba na Msanjila (2008), Kihore na wenzake (2008). Kutobainishwa kwa kategoria hiyo ni kusema kwamba wanaisimu hawa hawatambui kuwapo kwa kategoria ya vihusishi katika lugha ya Kiswahili.

Kwa upande wa Massamba na Msanjila (2008), wameainisha aina za maneno zifuatazo: nomino, viwakilishi, vivumishi, vitenzi, viunganishi, vielezi na viingizi. Katika uainishaji huu, kategoria ya kihusishi haikubainishwa moja kwa moja ingawa wamechopeka kama ni aina mojawapo ya viunganishi, yaani viunganishi vihusishi. Uainishaji huu unazua mkanganyiko ikiwa kuna uwezekano wa kuunganisha kategoria mbili (viunganishi na vihusishi) na kupata kategoria moja. Kihore na wenzake (2008) wameainisha aina saba za maneno ambazo ni: nomino, vivumishi, vitenzi, viwakilishi, viunganishi, vielezi na viingizi. Hata hivyo, wanajadili aina mojawapo ya viunganishi kuwa ni viunganishi vihusishi. Wanaeleza kuwa haya ni maneno yanayounganisha mahusiano ya uamilifu baina ya vitenzi vilivyotumika katika vishazi kwa upande mmoja na nomino kwa upande wa pili kuunda sentensi moja; kwa mfano, na, kwa, katika, kwenye, n.k., kama inavyoonekana katika mifano ifuatayo:

a. Mtoto anapigana **na** baba.
b. Mtoto anacheza **kwenye** matope.
c. Anaogelea **katika** maji marefu.
d. Juma amelala **kwa** mama yake.
e. Mwalimu amekuja **na** mtoto aliyefika kwake jana.

**Chanzo:** Kihore & *wenzake* (2008:169)

Katika mifano iliyotolewa hapo juu, hatuoni sababu ya kuita maneno hayo kuwa ni viunganishi vihusishi badala ya vihusishi. Hata tunapoangalia dhana ya viunganishi vihusishi tunapata mkanganyiko na kujiuliza ni kwa vipi neno liwe kiunganishi na kihusishi katika mazingira yaleyale na kwa dhima ileile. Kwa kawaida, viunganishi huunganisha dhana zenye hadhi sawa (Philipo, 2012). Kwa hiyo, maneno hayo tunaona kuwa ni vihusishi kwa kuwa yanahusisha sentensi (matendo) na vikundi nomino vya upande wa kulia mwa kikundi tenzi. Vipashio hivyo kimuundo havina hadhi sawa kwa kuwa kipashio kimoja ni sentensi na kingine ni kirai.

Besha (1997) anasema katika warsha ya kanda, juu ya kusahihisha *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (KKS) iliyoandaliwa na Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili tarehe 16-29/8/1993; lilitolewa pendekezo kuhusu uainishaji wa vihusishi kisarufi na kimaana na kuvipa hadhi ya vidahizo. Pendekezo hili lina umuhimu mkubwa katika kurekebisha yale yanayoelekea kuleta utenge katika matumizi ya Kiswahili. Vipo 'vineno' kadhaa ambavyo vimejikuta vimerundikwa chini ya kategoria moja kwa kukosa uainishaji sahihi wa kisarufi.

Kwa mfano, kategoria ya kiunganishi imebebeshwa mzigo mkubwa wa vineno ambavyo kimatumizi havisadifu kategoria hiyo, mathalani, vineno vinavyoundwa kwa -a unganifu (*ya, na, vya, kwa* n.k.).

Baadhi ya wanaisimu wanajenga hoja kuwa ingawa uchanganuzi wa vipengele vya lugha umekuwa ni jambo muhimu katika lugha zote, uainishaji wa maneno umekuwa ni shughuli binafsi au ya jumla ambapo mwainishaji huwa na lengo maalumu. Katika kazi hiyo, mwainishaji aeleze kanuni aliyoitumia katika uainishaji wake. Hali hiyo haiwabani wananadharia kuainisha maneno au kutoa maelezo ya kiufafanuzi au kiuzalishi (Aussant, 2013).

Pamoja na wataalamu kutofautiana katika uainishaji wa vihusishi, hatuwezi kuhukumu kuwa kategoria hiyo haipo katika lugha ya Kiswahili au tukubali tu kuwa maneno ya kategoria ya vihusishi yanaingiliana na maneno ya kategoria zingine. Kinachoonekana ni kuwa, baadhi ya wanaisimu kama vile Matinde (2012) na Habwe na Karanja (2004), pamoja na kukiri kuwa kategoria ya vihusishi ipo, bado wamekanganya maneno ya kategoria hiyo na maneno ya kategoria nyingine. Vilevile, wale wanaokataa kutokuwapo kwa kategoria ya vihusishi tunaona kama wanaleta mkanganyiko hasa pale wanapoweka maneno hayo katika kategoria ya viwakilishi ama kategoria ya vivumishi au kategoria ya viunganishi kama inavyoonekana kwa Kihore na wenzake (2008) na Massamba na Msanjila (2008). Makala hii inazingatia kuwa vihusishi ni kategoria mojawapo ya aina za maneno ya Kiswahili ambayo hujibainisha wazi dhidi ya kategoria zingine.

## 1.2. Dhana ya Vihusishi

Hartman (1972) katika Mgullu (1999) anaeleza kuwa kihusishi ni aina ya neno ambalo kwa kawaida haliambishwi viambishi vyovyote, litumiwalo pamoja na kikundi nomino ili kuonesha uhusiano uliopo baina ya kikundi husishi hicho na maneno mengine katika sentensi. Kwa maana kwamba, kihusishi huambatana na nomino na kuunda kikundi kihusishi. Kikundi kihusishi kinapokuwa katika sentensi huwa na dhima ya kuonesha uhusiano uliopo baina ya maneno mengine ndani ya sentensi husika. Naye Weber (1985) anaeleza kuwa kihusishi ni neno ambalo kwa kawaida hutumiwa na nomino au kiwakilishi na ambalo huzihusisha kisarufi nomino na viwakilishi hivyo na maneno mengine katika sentensi (Mgullu, 1999). Tunachoelezwa hapa ni kuwa kihusishi huambatana na ama nomino au kiwakilishi na dhima yake katika sentensi huwa ni kuonesha uhusiano

baina ya nomino au kiwakilishi kilichoambatana nacho na maneno mengine katika tungo. Vilevile, inaelezwa kuwa kihusishi ni neno linaloonesha uhusiano uliopo baina ya neno moja na neno au maneno mengine katika tungo na sentensi moja na nyingine (TATAKI, 2014).

Katika lugha ya Kiswahili, kuna wanaisimu kama vile Philipo na Kuyenga (2017) ambao wanaielezea dhana ya kihusishi kuwa ni ni kategoria ya kiuamilifu ambayo huonesha uhusiano wa kategoria zenye hadhi tofauti. Vihusishi katika lugha ya Kiswahili ni: “na”, “ya”, “kwa”, “za”, “la”, “cha” na “vya”. Haya ni maneno yanayoundwa na a-unganifu. A-unganifu ni aina ya kiambishi tamati kinachoambishwa kwenye kiambishi ngeli kwa ajili ya kuleta maana inayotakiwa kwenye upatanisho wa kisarufi baina ya makundi mbalimbali ya maneno. Wanaisimu hawa hawakuishia tu kuifasili dhana ya kihusishi bali wamebainisha kuwa vihusishi ni miongoni mwa maneno yanayotumika katika lugha ya Kiswahili.

Katika sehemu hii tumeona wanaisimu wakitofautiana katika kuainisha kategoria ya vihusishi. Kuna wanaisimu wanaovielezea vihusishi kama mojawapo ya kategoria ya maneno na wakati huohuo wanaweka pia maneno ya kategoria hii kama aina za maneno ya kategoria zingine. Aidha, kuna wale ambao hawajaweka wazi juu ya vihusishi kama kategoria lakini wanachopeka vihusishi katika kategoria zingine. Kuhitilafiana kwa wataalamu hutufikirisha ili kujua kama kategoria ya vihusishi ipo kama kategoria mojawapo ya maneno au ni maneno katika kategoria fulanifulani? Maumbo ya vihusishi yakoje na uamilifu wake katika tungo ni upi? Zaidi ya hayo, je, vihusishi huingiliana na maneno ya kategoria zingine katika tungo? Hivyo, tunaona kwamba kuna utata mkubwa kuhusiana na uainishaji wa vihusishi unaohitaji kutatuliwa kwa lengo la kuibainisha wazi kategoria ya vihusishi.

## 2.0 Methodolojia

Utafiti huu ulitumia mbinu ya uchanganuzi wa nyaraka kutoka katika maandiko ya wanaisimu wa lugha za kigeni sambamba na wa lugha ya Kiswahili. Uchanganuzi huo ulizingatia uainishaji wa kategoria ya vihusishi, aina za vihusishi, fasili, sifa na dhima ya vihusishi. Taarifa zilizotokana na uchanganuzi huo zimewasilishwa kwa kuzingatia ufanano au utofauti wake. Baadhi ya mifano ya data kutoka katika nyaraka hizo imenukuliwa na kutolewa ufafanuzi. Mbali na taarifa kutoka katika nyaraka hizo, mwandishi ameongeza baadhi ya kauli, sifa na aina za vihusishi;

hivyo, zisichanganywe na nukuu za mapitio ya maandiko. Aidha, sifa na dhima zilizobainishwa katika makala hii zinatoa vigezo vya msingi vya uainishaji wa kategoria ya vihusishi katika Kiswahili.

**3.0 Mjadala Kuhusu Uainishaji wa Vihusishi**

Kutokana na kuhitilafiana kwa wataalamu katika kuainisha kategoria ya vihusishi katika lugha ya Kiswahili, ni muhimu kuchunguza tena namna ya kuainisha kategoria ya vihusishi katika lugha hiyo. Pengine kwa kuwa vihusishi vina sifa za kisemantiki na kisintaksia zinazokaribia kufanana na viwakilishi au vivumishi, husababisha baadhi ya wataalamu kuchanganya maneno hayo katika kategoria tofauti na vihusishi. Landau (1984) akinukuliwa na Chuwa (1995) anasema wanaleksikografia wa kamusi za Kiswahili walikuwa hawashughuliki na vihusishi kama kategoria inayojitegemea. Wakati mwingine, waliviweka vihusishi katika kategoria ya viunganishi pasipo kuvichunguza kiundani kama vinafanya kazi sawasawa na viunganishi. Anaendelea kufafanua zaidi kuwa walitazama vihusishi kama maneno yasiyo na maana leksika. Vineno hivi si kwamba havina maana leksika, ila maana zake haziwezi kuelezeka kwa kufuata mfumo wa utoaji maana wa maneno ya kawaida katika lugha. Maana zake zinaelezeka kwanza kwa kubainisha kategoria zake na pili kwa kueleza wajibu vinavyotekeleza katika muundo wa sentensi. Maelezo hayo yanatupatia picha kwamba kuna utofauti wa namna ya kutazama vihusishi na maneno ya kategoria zingine. Maana ya vihusishi haikuwa wazi bali hutegemea dhima yake katika muundo wa sentensi.

Makala hii inapendekeza kuwa uainishaji wa vihusishi uzingatie vigezo mbalimbali kama vile kigezo cha kisintaksia, yaani kuzingatia mtawanyiko wake katika tungo, mnyumbuliko na dhima, kigezo cha kimofolojia na kigezo cha kisemantiki.

**3.1 Aina za Vihusishi**

Besha (1997) anasema kuwa uainishaji wa vipashio vya lugha ni msingi muhimu katika uchanganuzi wa muundo wa lugha hiyo. Hivyo, kila lugha ni lazima kuwa na vigezo vya wazi vitakavyosaidia katika kuainisha makundi ya maneno. Mwanasarufi wa lugha ya Kiswahili anaweza kujiuliza, kwa mfano, kuna aina ngapi za maneno katika lugha ya Kiswahili? Sio rahisi kupata majawabu ya haraka. Mwanasarufi wa Kiswahili anapaswa kuwa na misingi madhubuti ya uainishaji itakayomwezesha kutetea hoja zake. Yatbaz na wenzake (2012) wananukuu

wazo la Harris (1954) linalopendekeza kuwa maneno yanayotokea katika muktadha sawa huwa na maana na sifa za kisintaksia zinazofanana. Tafiti zinaonesha kuwa taarifa za mtawanyiko wa maneno ni kiashiria kizuri cha kutambua kategoria za maneno.

Baadhi ya wataalamu wamejadili aina mbalimbali za vihusishi. Habwe na Karanja (2004) wakimnukuu Kapinga (1985) wanadai kuwa kuna aina mbili za vihusishi: vile vinavyoundwa kwa kutumia mofimu –a unganifu na vile vinanyotokana na maneno yenye asili ya kigeni. Mfano wa vihusishi vya a-unganifu ni: kati ya, mbele ya, nyuma ya, juu ya na mifano ya vihusishi vinavyotokana na maneno ya kigeni ni hadi, tena, mpaka, tangu, kisha, halafu n.k. Pia, Matinde (2012) anajadili aina tano ya vihusishi navyo ni: vihusishi vya ukaribu, sababu, wakati, kiasi na a-unganifu. Katika makala hii, tumebainisha aina za vihusishi katika Kiswahili kwa kutumia kigezo cha mofolojia, sintaksia na semantiki.

Vigezo hivyo tunaona ni mwafaka katika kutatua mgongano wa kuchanganya kategoria ya vihusishi na kategoria zingine za maneno katika Kiswahili ambao, kwa maoni yetu, tunaona unachangiwa na matumizi ya kigezo kimoja tu cha uainishaji wa maneno.

**a) Kigezo cha Kimofolojia**

Mofolojia ni taaluma ya isimu inayoshughulikia uchambuzi na uchunguzi wa kanuni na mifumo inayohusu upangaji wa mofimu mbalimbali ili kuunda maneno katika lugha (Massamba, 2004). Kwa kutumia kigezo cha kimofolojia, tunapata kuona kuwa vihusishi ni kundi la maneno yenye sifa zifuatazo: kwanza, vihusishi huundwa na maneno ambayo hayaambishwi yaani vihusishi ni maneno funge. Pia, kimuundo, vihusishi huundwa na neno moja kama vile, *hadi, kabla, tena, na* n.k., na vingine huwa na muundo changamano yaani huwa na neno zaidi ya moja mfano, *kandokando ya, chini ya, mbele ya, kabla ya* n.k. Hivyo, kutokana na kigezo cha kimofolojia tunapata aina mbili za vihusishi nazo ni vihusishi huru ambavyo huundwa na neno moja pekee na aina ya pili ni vihusishi changamano ambavyo huundwa na neno zaidi ya moja.

**b) Kigezo cha Kisintaksia**

Sintaksia ni taaluma ya isimu inayochanganua mpangilio wa uhusiano wa maneno na vipashio katika tungo (Massamba, 2004). Kigezo cha kisintaksia huonesha mtawanyiko wa maneno au nafasi ya neno katika

sentensi. Vihusishi katika Kiswahili huweza kuchukua nafasi ya mwanzo, kati au mwisho.

Nafasi ya mwanzo; vihusishi huweza kuchukua nafasi ya mwanzo wa sentensi katika sentensi ambazo zina nomino ya kiima kapa, kwa mfano,

i. **Cha** moto amekiona.
ii. **La** kijiji limekamilika.
iii. **Ya** shuleni imeanza.

Nafasi ya kati; vihusishi hujitokeza baada ya nomino ya kiima au kivumishi cha nomino ya kiima; kwa mfano,

i. Kiti **cha** Rais kinagombaniwa.
ii. Mti **wa** matunda umekauka.
iii. Lugha yetu **ya** Kiswahili inazidi kukua.
iv. Mwalimu wako **wa** sayansi anakusalimu.

Nafasi ya mwishoni; vihusishi hujitokeza baada ya kitenzi au nomino ya kikundi tenzi kama vile:

i. Mwanafunzi anasoma **kwa** shida.
ii. Makala imeandikwa **na** Mswahili.
iii. Mtoto ameshika mti **wa** matunda.
iv. Tulitimua mbio **hadi** nyumbani.
v. Juma atakuja **nalo.**

Kigezo cha kisintaksia kinatuonesha kuwa vihusishi, mara nyingi, hufuatwa na nomino au kiwakilishi kama vile: *kwa mjomba, la moto, za kwetu, la kwake* n.k. Pia, huweza kutanguliwa na nomino, viwakilishi, vivumishi, vibainishi, vitenzi na vielezi na kufuatiwa na nomino au kiwakilishi. Hii ina maana kwamba, sio rahisi katika muundo wa sentensi ya Kiswahili kuanza na kihusishi au kuishia na kihusishi.

**c) Kigezo cha Kisematiki**

Semantiki ni taaluma ya isimu inayojishughulisha na uchunguzi na uchambuzi wa maana za maneno au tungo katika lugha (Massamba, 2004). Kigezo cha kisemantiki kinaweza kutumika kupata aina za vihusishi kwa kuangalia dhima za maneno hayo katika tungo. Kwa ujumla, kutokana na dhima za vihusishi tunapata aina zifuatazo za vihusishi:

a. Vihusishi vya ukaribu: ni maneno yanayoonesha uhusiano uliopo baina ya neno hilo na nomino inayotaja kitu, mtu, hali matendo au

mahali; kwa mfano, chini ya, juu ya, mbele ya, kandokando ya, mbali na, pamoja na, nje ya n.k.
Mfano:
i. Embe limeanguka **chini ya** mti.
ii. Kunguru amerukia **juu ya** nyumba.
iii. Anakaa **mbali na** mimi.
iv. Wamejenga **kandokando ya** bahari.
v. Wazazi wanaishi **pamoja na** watoto.

b. Vihusishi vya wakati: ni maneno yanayoonesha uhusiano uliopo baina ya matendo au matendo na nomino; kwa mfano, kabla ya, baada ya, mwishoni mwa, katikati ya n.k. Mfano:
i. Wakoloni waliondoka **kabla ya** uhuru.
ii. Tunanawa **baada ya** kula.
iii. Maswali hutolewa **mwishoni mwa** kipindi.
iv. Wanafunzi wengi hawasomi **mwanzoni mwa** muhula.
v. Askari waliingia **katikati ya** mazishi.

c. Vihusishi vya sababu: haya ni maneno yanayodokeza sababu au dhumuni la kufanyika kwa tendo fulani, kwa mfano, *kwa sababu, kwa ajili ya, kwa kusudi la, kwa lengo la, kwa* n.k.
Mfano:
i. Watu wanadhoofu **kwa sababu ya** njaa.
ii. Nitaangamia **kwa ajili** yako.
iii. Kunywa maji **kwa** afya yako.
iv. Nimewaita **kwa** lengo la kuwapa taarifa muhimu.
v. Ninawazawadia gari **kwa** kusudi la kuwahamasisha utendaji mzuri.

d. Vihusishi vya ala: ni maneno yanayoonesha uhusiano baina ya tendo na kifaa au kitu kilichotumika katika utekelezaji wa tendo hilo. Katika lugha ya Kiswahili, kihusishi "kwa" hutumika zaidi.
Mfano:
i. Amekata nyama **kwa** kisu.
ii. Wamechapwa **kwa** bakora.
iii. Anaitikia **kwa** kichwa.
iv. Anatoa kinyesi **kwa** mkono.
v. Majambazi waliuawa **kwa** risasi.

e. Vihusishi vya umiliki: ni maneno yanayodokeza umiliki wa kitu, mahali, sehemu au hali na kitu kingine. Vihusishi vinavyoingia katika kundi hili ni mwa, cha, ya, la, vya, wa, mwenye n.k.
Mfano:

i. Gari **la** mjomba linapendeza.
ii. Utumbo **wa** mbuzi haupendwi sana.
iii. Chakula **cha** wageni kiko tayari.
iv. Mama **mwenye** nyumba ni mpole sana.
v. Kusini **mwa** Tanzania kuna Wamatengo.

f. Vihusishi vya chanzo/ukomo: ni vihusishi ambavyo mara nyingi huonesha uhusiano uliopo baina ya kuanza au kuishia kwa tendo na maneno mengine. Vihusishi hivyo ni *tangu, toka, hadi, mpaka* n.k.
Mfano:
i. Mtoto amelia **tangu** usiku wa manane.
ii. Wameondoka **toka** asubuhi.
iii. Sitakubali **hadi** kieleweke.
iv. Nitachapa kazi **mpaka** niitwe nyumbani.
v. Walipendana **tangu** kuoana **hadi** kifo..

g. Vihusishi vya mahali: ni maneno yanayoonesha uelekeo wa tendo au sehemu; mfano, ndani ya, katikati ya, kwa, kwenye, n.k.
Mfano:
i. Kapai anaishi **kwa** kaka yake.
ii. Babu ameweka pesa **ndani ya** mtungi.
iii. Watoto wamekwenda **kwenye** sherehe.
iv. Wezi wamekutwa **katikati ya** pori.

h. Vihusishi utendi: ni maneno yanayodokeza uhusiano baina ya tendo na mtendaji. Kihusishi kinachotumika katika lugha ya Kiswahili ni "na".
Mfano:
i. Stela amepigwa **na** Stan.
ii. Makala imeandikwa **na** mwalimu wake.
iii. Wanafunzi wamekutwa **na** mlinzi.
iv. Kikao kiliongozwa **na** wazee.
v. Barabara imejengwa **na** Wachina.

Katika sehemu hii tumeainisha vihusishi kwa kutumia vigezo mbalimbali. Hivyo, mifano ya vihusishi iliyotolewa inatoa picha kuwa vihusishi ni kundi la maneno yanayojibainisha wazi dhidi ya maneno ya kategoria zingine kiasi kwamba, kwa kutumia vigezo tofautitofauti vya uainishaji wa maneno, wanaisimu wanafanikiwa kuainisha maneno hayo kwa namna ambayo haitaleta mkanganyiko unaotokana na kuweka vihusishi katika kategoria zingine za maneno.

**4.0 Hitimisho**

Makala hii imebainisha wazi kuwa kategoria ya vihusishi imekuwa ikitafsiriwa na kufasiliwa tofautitofauti na wanaisimu. Hali hiyo imesababisha maneno ya kategoria hii kuwekwa katika kapu la maneno ya kategoria zingine kwa madai ya kufanana na maneno hayo kidhima. Vilevile, baadhi ya wanaisimu wameacha kuainisha kategoria ya vihusishi katika uainishaji wao. Tatizo hili linajitokeza kwa sababu ya mazoea ya jumlajumla ya kuelewa dhana ya vihusishi, maumbo dhahiri ya vihusishi na dhima zake katika tungo. Katika kutatua tatizo hili, makala hii imetambua umuhimu wa tabia ya maneno katika tungo ya kuingiliana na kuathiriana kimaana na kikazi. Makala inapendekeza kuainisha vihusishi kwa kutumia kigezo cha kisintaksia, yaani: mfuatano wake katika tungo, mnyambuliko wake, na kazi zake kisarufi, kigezo cha kimofolojia na kigezo cha kisemantiki. Hii itasaidia kuondoa utata na mkanganyiko wa aina za maneno uliopo sasa.

**Marejeleo**


Aussant, E. (2013). To Classify Words: Western and Indian Grammatical Approaches. Selected Papers Presented at the Seminar on Sanskrit Syntax and Discourse Structures, Université Paris Diderot.

Besha R. (1997). Nomino za Kiswahili: Misingi ya uainishaji. *Kioo cha Lugha*. 2, 1-14.

Chuwa, R. (1995). Dhima ya kamusi katika kubainisha matumizi ya vihusishi (Mfano: Kihusishi KWA). *Nordic Journal of African Studies.* 4 (2), 73-79.

Habwe, J. na Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Kihore, Y. Massamba, D. na wenzake Msanjila, Y. (2008). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu* (*SAMAKISA*): *Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam:TUKI.

Kihore, Y.M. (1996b). *Kiswahili OFC 5*: *Kozi za Maandalizi*. Dar es Salaam: The Open University of Tanzania.

Massamba, D .P.B. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.

Massamba, D.P.B na wenzake. (1999). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu* (*SAMIKISA*): *Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: TUKI.

Matinde, R. S. (2012). *Dafina ya Lugha*: *Isimu na Nadharia* (*Kwa Sekondari*, *Vyuo vya Kati na Vyuo Vikuu*. Mwanza: Serengeti Educational Publishers Ltd.

Mgullu, R. (1999). *Mtalaa wa Isimu*: *Fonetiki*, *Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers Ltd.

Philipo Z. T. na Kuyenga F. E. (2017). *Sintaksia ya Kiswahili*: *Nadharia za Kisintaksia na Uchanganuzi wa Kiswahili*. Dar es Salaam: Karljamer Publishers Limited.

Philipo, Z. T. (2012). Tofauti baina ya vivumishi na vibainishi katika lugha ya Kiswahili. *Kioo cha Lugha*.13, 125-143.

TATAKI (2014). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.

Yatbaz, M. (2012). Learning syntactic categories using paradigmatic representations of word context. *EMNLP-CoNLL*. 1, 940–951.